



**THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN
AFRICA**

A. M. E. C. E. A.


P.O. Box 62157, 00200
Nairobi – KENYA
Telephone: 891601-6
Fax: 254-20-891084
E-mail: academics@cuea.edu

**SHAHADA YA KWANZA YA SANAA KATIKA
KISWAHILI NA MAWASILIANO**

**Imewasilishwa kwa Tume ya Elimu ya Juu,
NAIROBI**

This Degree Programme Was
approved by the Commission for
Higher Education on:

22 MAR 2012


.....
Authorized Signature

Februari, 2012

2.0 Mtalaa wa Kozi Hii

2.1 Anwani ya Kozi Pendekezwa

Shahada ya Kwanza katika Kiswahili na Mawasiliano

2.2 Falsafa ya Kozi

Kozi hii inanuiwa kuwahitimisha wasomi wenye maarifa ya kimsingi katika Isimu, Fasihi na Mawasiliano na ambao wana maadili ya kuitumikia jamii kwa haki na ukweli katika misingi ya maadili ya Kikristo.

2.3 Umuhimu wa Kozi Hii

Uanzishaji wa kozi hii unalenga kukidhi mahitaji makubwa ya wataalamu wa isimu, fasihi, pamoja na mawasiliano katika eneo la Mashariki mwa Afrika. Uchunguzi uliotangulia maandalizi ya kozi hii ulibainisha uhaba mkubwa wa wataalamu katika nyanja hizi.

2.4 Madhumuni ya Jumla

Kozi ya B.A. (Kiswahili na Mawasiliano) inanuiwa kufundisha wataalamu wenye ubunifu, ukakamavu, ujuzi na uwezo wa kujiunga na sekta mbalimbali za uchumi na kijamii zinazojihusisha na lugha na mawasiliano ili kutoa mchango thabiti.

CUEA ni chuo cha ya Kikatoliki cha masomo ya juu kilichoasisiwa na kuendeshwa kwa msaa wa Jumuiya Wanachama wa Muungano wa Maaskofu wa Afrika Mashariki (AMECEA). Kwa kariha ya maneno ya Yesu Kristo, "Wakifu katika Ukweli (Yh 17:17)", chuo kinalenga kukuza utafiti wa kisayansi, ufundishaji bora na hudumu stahiki ya jamii kwa kusudi la kuimarisha maisha ya Ukristo.

Katika misingi ya neno la Mungu, desturi inayodumu na mafundisho bia ya kanisa na ya kimaeneo; chuo kinatoa kozi ambazo zimeundwa kuwaandaa wanaostahili kwa kanisa na jamii.

Aidha, kinalenga kukuza mahusiano na ushirikiano na vyuo vingine vikuu kwa lengo la kujenga jamii bora ya wanadamu.

2.5 Malengo Mahsusi

Kozi ya B.A. katika Kiswahili na Mawasiliano inalenga kutoa fursa mahsusi kwa masomo ya kinadharia na masomo tumikizi. Inawatayarisha walengwa:

- i) Kutekeleza majukumu ya kiusomi na kimawasiliano katika Kiswahili ili kuchangia maendeleo ya kitaifa, kimataifa na ulimwengu kwa jumla.
- ii) Kuendesha shughuli mbalimbali zinazohusiana na lugha na mawasiliano katika sekta mbalimbali.
- iii) Kutumia ujuzi walioupata katika kufanya utafiti wa kisayansi kwa minajili ya kukabiliana na changamoto katika nyanja zao za usomi na za kikazi.
- iv) Kufanikisha mawasiliano baina yao na wanajamii, na pia maingiliano ya kijamii kwa kutumia maarifa ya kozi hii.

2.6 Mtindo wa Ufundishaji

Ufundishaji utafanywa kwa njia ya wahadhiri kukutana ana kwa ana na wanafunzi chuoni.

2.7 Mahitaji ya Shahada Hii

2.7.1 Masharti ya Usajili

- a) Masharti yanayohusu shahada za kwanza katika Chuo Kikuu yatatumika.
- b) Masharti yanayohusu shahada za kwanza katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii yatatumika.
- c) Idara itasajili:
 - i) Wanafunzi walio na alama ya C+ na zaidi katika Kiswahili katika mtihani wa KCSE au kiwango sawa na hicho watasajiliwa katika kozi ya kipindi cha miaka minne.
 - ii) Wanafunzi waliofuzu katika kiwango cha “Principal” katika mtihani wa “A level” au kiwango sawa na hicho watasajiliwa katika kozi ya miaka mitatu.
 - iii) Wanafunzi waliofuzu na ‘credit’ au zaidi katika Kiswahili katika kiwango cha diploma au kiwango sawa na hicho, watasajiliwa katika kozi ya miaka miwili.

2.7.2 Mahitaji ya Kozi

Kwa jumla kozi hii itamhitaji mwanafunzi ahudurie madarasa pamoja na mafunzo ya nyanjani ambayo yatatolewa katika hali halisi ya utendaji kazi katika mashirika mbalimbali. Aidha, itamhitaji mwanafunzi kufanya kozi zinazofanywa na wanafunzi wote chuoni (GS) kwa sababu zinawapa wanafunzi maarifa mbalimbali na maadili ya kijamii.